MAIR

Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji MKUKUTA - 2006/2007

Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA

Mwaka 2001, Serikali iliandaa Mfumo wa Ufuatiliaji Umaskini kwa ajili ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Mfumo huo ulipitiwa na kuboreshwa mwaka 2005/06 ili uweze kutumika kufuatilia MKUKUTA ambao ni mkakati mpana zaidi na wenye kuzingatia matokeo zaidi kuliko Mkakati wa awali wa Kupunguza Umaskini. Mfumo wa ufualiaji uliopitiwa na kuboreshwa uliidhishwa mwaka 2006 na unajulikana kama Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA. Mfumo huu unaongozwa na waraka wa Mpango Mkuu wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA. Kiini cha Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA ni makundi matatu ya kiufundi yafuatayo:

Kundi la Kiufundi la Utafiti na Uchambuzi

Kundi hili linawajibika na uchambuzi wa takwimu na kuratibu utafiti wa kitaifa ambao hutoa taarifa kwa ajili ya watunga sera na wadau wengine.

Kundi la Kiufundi na Tafiti na Takwimu za Kila Siku za Kiutawala

Kundi hili linawajibika na ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu zitokanazo na tafiti za kitaifa na zitokanazo na utendaji wa kila siku wa serikali. **Kundi dogo la takwimu za kila siku za kiutawala** linaandaa Mpango Mkuu wa Takwimu Tanzania, wenye lengo la kuboresha takwimu ili kusaidia ufuatiliaji na tathmini. Mpango huo unatoa mwelekeo wa kimkakati wa kuimarisha uwezo wa kitakwimu na michakato ya uundaji wa sera, mipango na utoaji maamuzi yenye kuzingatia ushahidi wa kitakwimu. **Kundi dogo la utafiti** linawajibika na tafiti za kitaifa kama vilivyobainishwa kwenye kalenda ya Mpango Mkuu wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA.

Kundi la Kiufundi la Mawasiliano

Kundi hili linawajibika na uhabarishaji wa (a) Muundo wa MKUKUTA (b) matokeo ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA. Hii husaidia kuchochea mijadala na midahalo miongoni mwa wadau na kuunga mkono utekelezaji wa MKUKUTA

Shughuli Zinazoendelea

- Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA unahusisha kuunganisha taarifa mbali mbali za utekelezaji kutoka kwenye ofisi za serikali na kuzijumuisha

na tafiti zinazojitegemea pamoja na kazi za uchambuzi. Utoaji wa taarifa unapaswa kufanyika kupitia: (a) Ripoti ya mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA, yaani MAIR (b) Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Watu.

- Taarifa za ofisi za serikali za utekelezaji za robo mwaka zitahusishwa na matokeo ya kila nguzo ya MKUKUTA kupitia Mfumo Mpya wa Utoaji Taarifa za MKUKUTA (RIMKU), na pia kupitia Mapitio ya Kisekta, Mapitio ya Matumizi ya Umma na Taarifa za ukaguzi.

- Serikali imedhamiria kuoanisha mifumo mbali mbali ya utoaji taarifa ili kuimarisha uhusisano wa jumla na MKUKUTA na baina ya Mipango, Bajeti na mifumo ya utoaji taarifa. Mifumo ya kompyuta imekuwa ikitumika kusaidia kufanikisha mchakato huu.

Changamoto na Mambo Tuliyojifunza

- Muundo wa MKUKUTA wa kuzingatia matokeo unahusisha wadau wengi zaidi kuliko Mkakati wa awali wa Upunguzaji Umaskini. Kwa hali hiyo; unahitajika (a) mfumo madhubuti zaidi wa Ufuatiliaji na Utoaji taarifa (b) Muunganiko bayana baina ya serikali na wadau wengine muhimu, na (c) Uimarishaji wa michakato ya uwajibikaji.

- Muunganiko baina ya serikali na wadau wengine umebaki kuwa dhaifu. Bado kuna tofauti baina ya viashiria vinavyotumika kwa shughuli za MKUKUTA, na pale vinapokuwepo, katika muundo wa utendaji wa serikali. Upanuzi wa viashiria hadi 84 unamaanisha kwamba kazi yenye mpangilio mzuri zaidi inahitajika kufanywa.

- Pamoja na mafanikio makubwa ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA, unategemea msaada kutoka kwa Wabia wa Maendeleo. Hali hii inatishia uendelevu wa mfumo huu.

- Mahudhurio ya Vikao vya Makundi ya Kiufundi yamekuwa si mazuri, hivyo kuathiri utekelezaji wa kazi zilizopangwa. Moja ya sababu za mahudhurio hafifu ni kwamba kazi za makundi hayo hazijajumuishwa kwenye kazi za kawaida za taasisi wanakotoka. Hali hii inapelekea matarajio ambayo hayawezi kufikiwa. Inapendekezwa kuwa wajumbe wa makundi haya washirikishwe katika utendaji wa baadhi ya kazi badala ya kuwa washauri tu

Hatua za kuchukua

- Juhudi zitaendelea kuaonisha Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA kwenye taasisi za serikali ili kuhakikisha utoaji taarifa wa kiwango cha juu na utoaji maamuzi ulio bora zaidi

- Kazi za Ufuatiliaji na Tathmini kwenye ofisi za serikali zitabainishwa ili kuzioanisha na Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA. Hii itahusisha uandaaji wa sera ya Ufuatiliaji na Tathmini sambamba na ujengaji uwezo katika ngazi zote.

- Utafiti umefanyika ili kuondoa Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA kutoka kwenye utegemezi wa Mfuko wa Ufadhili na kwenda katika kuujumuisha kwenye Bajeti ya kitaifa. Serikali itatekeleza pole pole mapendekezo ya utafiti huo.

- Kamati maalum ya serikali na Wabia wa Maendeleo imeundwa ili kubainisha masuala muhimu ikiwa ni pamoja na ugharimiaji na uimarishaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA. Masuala haya yatashughulikiwa katika kipindi cha mpito kitakachoishia mwaka 2012

- MKUKUTA unaozingatia Nguzo na mtazamo wa matokeo hutegemea mchango wa washiriki kutoka sekta mbali mbali katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Hii inahitaji kuifanyia maboresho baadhi ya michakato inayoendelea ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo mkabala ulioratibiwa na kuoanishwa vizuri kutoka watu mbali mbali wanaohusika. Kuwepo kwa mfuatanisho unaotokea kwa wakati muafaka ni muhimu sana.

- Mwaka 2006/07 iliundwa Timu Maalumu ya Wizara mbalimbali kwa ajili ya Mipango, Bajeti na Utoaji taarifa. Lengo la timu hii lilikuwa ni kuoanisha taratibu za serikali za utoaji taarifa, ufuatiliaji na tathmini. Yamepatikana mafanikio ya kuridhisha katika hili.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Wizara ya Fedha na Uchumi,
S..L.P. 9111, Dar Es Salaam
Simu: +255 2111174, Fax 21103226
Barua Pepe: mkukuta@gmail.com; Tovuti: www.povertymonitoring.go.tz